

القرآن الحكيم

QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

39. Na (vile vile) Karuni na Firauni na Hamana (waliangamizwa); na hakika aliwajia Musa kwa miujiza waziwazi, lakini walijivuna katika ardhi, lakini hawakuweza kumshinda (Mwenyezi Mungu).

40. Basi kila mmoja tulimtesa kwa sababu ya dhambi zake; miongoni mwao wako tuliowapelekea kimbunga cha changarawe; na miongoni mwao wako waliotolewa roho kwa ukelele mkubwa (uliopigwa na Jibrili); na miongoni mwao wako tuliowadidimiza ardhini; na miongoni mwao wako tuliowagharikisha. Na hakuwa Mwenyezi Mungu Mwenye kuwadhulumu, lakini walikuwa wakijidhulumu (wenyewe) nafsi zao.

41. Mfano wa wale waliofanya waungu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ni kama mfano wa buibui ajitandiaye nyumba (yake ili imhifadhi, nayo haimhifadhi na lolote); na bila shaka nyumba iliyo dhaifu kuliko zote ni nyumba ya buibui; laiti wanalijua!

42. Kwa yakini Mwenyezi Mungu anajua huko kuabudu kwao vyengine wakamuacha yeye (Mwenyezi Mungu); naye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

43. Na hiyo mifano tunawapigia watu; na hawaifahamu ila wajuao.

44. Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa haki. Kwa hakika katika hayo zimo hoja (dhahiri) kwa wanaoamini.

45. Soma ulioletewa Wahyi (uliyofunuliwa) katika Kitabu (hiki ulicholetewa) na usimamishe Sala. Bila shaka Sala (ikisaliwa vilivyo) humzuiliya (huyo mwenye kusali na) mambo machafu na maovu, na kwa yakini kumbuko la Mwenyezi

وَقَارُونَ وَفِرْعَوْنَ وَهَامَانَ وَقَدْ
جَاءَهُمْ مُوسَى بِالْبَيِّنَاتِ فَاسْتَكْبَرُوا
فِي الْأَرْضِ وَمَا كَانُوا سَاقِينَ

فَكُلًّا أَخَذْنَا بِذُنُوبِهِمْ فَمِنْهُمْ مَنْ أَرْسَلْنَا عَلَيْهِ
حَاصِبًا وَمِنْهُمْ مَنْ أَخَذَتْهُ الطَّيْفَةُ وَمِنْهُمْ مَنْ
خَسَفْنَا بِهِ الْأَرْضَ وَمِنْهُمْ مَنْ أَغْرَقْنَا وَمَا
كَانَ اللَّهُ لِيُظْلِمَهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ
يُظْلِمُونَ

مَثَلُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَاءَ
كَثَلِ الْعَنْكَبُوتِ إِذَا أَخَذَتْ بَيْتًا وَإِنَّ أَوْهَنَ
الْبُيُوتِ لَبَيْتُ الْعَنْكَبُوتِ لَمَكُونًا يُعْلَمُونَ
إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُدْعُونَ مِنْ دُونِهِ مِنْ
شَيْءٍ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

وَتِلْكَ الْأَمْثَالُ لَضَرِبَ لَهَا لِلنَّاسِ وَمَا يَعْقِلُهَا
إِلَّا الْعَالِمُونَ

خَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ
إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِلْمُؤْمِنِينَ

أَتْلُ مَا أُوْحِيَ إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ وَأَقِمِ الصَّلَاةَ
إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَلَذِكْرُ اللَّهِ

41. Hapa ni kama vile tunavyosema kila siku kuwa wa kuombwa akaweza (a) kuondoa mabaya, au (b) kuleta mema ni Mwenyezi Mungu tu peke yake si Sharifu wa Mtaa wa Mackinon Road wala Sharifu wa mtaa wa Sharifu Musa wala Shekhe wa mtaa wa Mtoni wala Shekhe wa mtaa wa Fujoni, wala mzimu wa Baa Farjallah wala pepo wa Vura wala wengineo wala mengineyo.

Mambo yote ni ya Mungu
Ndiye Pweke Mwenye Quwa

Atakalo ndilo huwa
Mwenye amri na shani.

43. Hapa Aya hii — kama Aya ya 22 ya *Suratur Rum* na ya 15 ya *Suratul Ankabuut* na nyinginezo — inahimiza kusoma kwani kwa kusoma ndipo utapofahamu hayo ambayo Mwenyezi Mungu na Mitumewe wanayasema. Na kuyajua hayo na kuyafwata ndio kutengenekeza duniani na akhera.

45. Baadhi ya wakubwa wa Dhikiri wanaotaka kupoteza watu wanalifasiri vibaya — makusudi — hili tamko la *Waladhikrullahi Akbar*. Wanasema dhikiri ndiyo bora kuliko Sala. Khiari yao. Watachukua mizigo yao na mizigo ya hao wawapoteza. Katika Uislamu — baada ya mtu kuwa Mwislamu — hapana amali bora kuliko Sala na ndiyo farka baina ya Uislamu na ukafiri. Basi, khiari yao; nawapoteze watu.

Mungu (lililomo ndani ya Sala) ni jambo kubwa kabisa (la kumzuilia mtu na mabaya). Na Mwenyezi Mungu Anajua mnayoyatenda.

46. Wala msibishane na watu waliopewa Kitabu (kabla yenu) ila kwa yale (majadiliano) yaliyo mazuri, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: "Tunaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu, na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja; nasi ni wenye kunyenyekea kwake."

47. Na namna hivi Tumekuteremshia Kitabu (hiki cha Qurani); basi wale Tuliowapa Kitabu (kabla ya hiki kama Tawrati na Injili wanakiamini (hiki kitabu ulichoteremshiwa kwani hakipingani na hivyo walivyoteremshiwa); na miongoni mwa hawa (Waarabu wasiokuwa na kitabu chochote) wako wanaokiamini; na hawazikatai Aya zetu isipokuwa wale wanaotaka kuficha haki.

48. Na hukuwa mwenye kusoma kitabu chochote kabla ya hiki, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume, (ingekuwa hivyo) wangepanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki).

49. Bali hizi ni Aya waziwazi (zinazokubaliwa) katika vifua vya wale waliopewa ilimu, na hawazikatai Aya Zetu isipokuwa madhalimu (wa nafsi zao).

50. Na walisema: "Mbona hakuteremshiwa miujiza kutoka kwa Mola wake?" Sema: "Miujiza iko Kwake Mwenyezi Mungu tu, (akitaka atakuteremshieni na kama hataki basi), nami hakika ni Mwonyaji Mbainishaji (dhahiri tu)."

51. Je, hayakuwatosha ya kwamba Tumekuteremshia Kitabu hiki wanachosomewa? Bila shaka katika hayo muna rehema na mauidha kwa watu wanaoamini.

52. Sema: "Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Shahidi baina yangu na nyinyi. Anajua yaliyomo katika mbingu na Ardhi. Na wale wanaokubali batili na kumkufuru Mwenyezi Mungu, hao ndio wapatao hasara."

اَكْبَرُ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ﴿٥٠﴾

وَلَا تُجَادِلُوا أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ۚ
إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ وَقُولُوا آمَنَّا بِالَّذِي أُنْزِلَ
إِلَيْنَا وَأُنْزِلَ إِلَيْكُمْ وَالْهِنَا وَالْهَكْمُ وَاحِدٌ
وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿٥١﴾

وَكَذَٰلِكَ أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ فَالَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ
يُؤْمِنُونَ بِهِ وَبِهِ هُوَ الَّذِي يُؤْمِنُ بِهِ، وَمَا يَجْحَدُ
بِآيَاتِنَا إِلَّا الْكَافِرُونَ ﴿٥٢﴾

وَمَا كُنْتَ تَتْلُو مِنْ قَبْلِهِ مِنْ كِتَابٍ وَلَا تَخُطُّهُ
بِإَمِينِكَ إِذْ أَرْسَلْنَا الْمُبْتَغُونَ ﴿٥٣﴾

بَلْ هُوَ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ فِي صُدُورِ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ
وَمَا يَجْحَدُ بِآيَاتِنَا إِلَّا الظَّالِمُونَ ﴿٥٤﴾

وَقَالُوا لَوْلَا أُنْزِلَ عَلَيْهِ آيَاتٌ مِنْ رَبِّهِ قُلْ
إِنَّمَا الْآيَاتُ عِنْدَ اللَّهِ وَإِنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ مُبِينٌ ﴿٥٥﴾

أَوَلَمْ يَكْفِهِمْ أَنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ
ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَرْحْمَةً وَذِكْرًا لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٦﴾

قُلْ كَفَىٰ بِاللّٰهِ بَيِّنًا وَبَيِّنَاتٍ شَهِيدًا يَعْلَمُ مَا فِي
السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ وَالَّذِينَ آمَنُوا بِالْبَاطِلِ وَكَفَرُوا
بِاللّٰهِ ۚ أُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٥٧﴾

48. Mwenyezi Mungu amewataka wasiokubali kuwa Qurani ni maneno Yake walete Sura moja mfano wa Sura za Qurani (2:23). Ikiwa wao wameshindwa, jee aliwezaje Mtume Muhammad aliyekuwa hajui kusoma wala kuandika? Bila shaka Qurani ni maneno ya Mwenyezi Mungu Mwenyewe.

51. Kuonyesha kuwa hakuna muujiza mkubwa na shahada kamili ya ukweli wa Uislamu kuliko hii Qurani isiyoweza kugunduliwa na kosa wala kutiwa kombo kwa lolote.

53. Na wanakuomba adhabu ifike upesi. Na kama pasingaliwekwa wakati maalumu (wa kuja adhabu, basi) adhabu ingaliwajia (sasa hivi). Na kwa yakini itawajia kwa ghafla, na hali ya kuwa hawana habari.

54. Wanakuhimiza adhabu (ije upesi). Na hali ya kuwa Jahanamu itawazunguka makafiri.

55. Siku itakapowafunika adhabu (hiyo) kutoka juu yao na kutoka chini ya miguu yao, na Atasema: "Onjeni (jaza ya) yale mliyokuwa mkitenda."

56. "Enyi waja Wangu mlioamini! Kwa yakini ardhi Yangu ina wasaa, (mnaweza kwenda nchi nyingine kama hampati fursa ya kufuata dini yenu katika nchi yenu); basi Mimi tu muniabudu."

57. Kila nafsi itaonja mauti, kisha mtarudishwa Kwetu.

58. Na ambao wameamini na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Tutawakalisha katika maghorofa ya Peponi mpitamo mito mbele yake, wakae humo milele. Ni mwema ulioje ujira wa watendao (mema):

59. Ambao walisubiri na wakamtegemea Mola wao.

60. Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao; Mwenyezi Mungu Huwaruzuku wao na nyinyi pia: naye ndiye Asikiaye, Ajuaye.

61. Na kama ukiwauliza, "Ni nani aliyeumba mbingu na ardhi na akalitiisha jua na mwezi?" Bila shaka watasema, "Mwenyezi Mungu." Wapi basi wanakogeziwa?

62. Mwenyezi Mungu Humkunjulia riziki Amtakaye katika waja Wake na Humdhikishia. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

63. Na ukiwauliza: "Ni nani ateremshaye maji mawinguni na kuihuisha ardhi baada ya kufa kwake?" Bila shaka watasema: "Mwenyezi Mungu." Sema: "Basi shukurani yote anastahiki Mwenyezi Mungu." Lakini wengi katika wao hawafahamu.

64. Na hayakuwa maisha haya ya dunia ila upuzi na mchezo; na nyumba ya akhera ndiyo maisha hasa: laiti wanalijua!

65. Na wanapopanda katika vyombo (wakafikwa na misukosuko), humuomba Mwenyezi

وَيَسْتَعِجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ ۖ وَلَوْ لَا أَجَلٌ مُّسَمًّى لَّجَاءَهُمُ الْعَذَابُ ۖ وَلِيَأْتِيَنَّهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٣﴾

يَسْتَعِجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ ۖ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ بِالْكَافِرِينَ ﴿٥٤﴾

يَوْمَ يُعْصَمُ الْعَذَابُ مِنَ قُوَّتِهِمْ وَمِنَ تَحْتِ أَجْلِهِمْ وَيَقُولُ ذُوقُوا مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٥٥﴾ يُعَادِلُ فِي الَّذِينَ آمَنُوا لَنْ أَرْضَىٰ وَاسِعَةً قُلُوبًا ۖ فَاعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

كُلُّ نَفْسٍ ذَاقَةُ الْمَوْتِ ثُمَّ إِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ﴿٥٧﴾ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَنُبَوِّئَنَّهُم مِّنَ الْجَنَّةِ غُرَفًا تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۖ نِعْمَ أَجْرُ الْعَامِلِينَ ﴿٥٨﴾

الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٥٩﴾

وَكَايْنٍ مِّنْ دَابَّةٍ لَا يُلْجَأُ رِزْقُهَا ۖ اللَّهُ يُرْزِقُهَا وَيَايَاكُمْ ۚ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٦٠﴾

وَلَكِنْ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَصَوَّرَ النَّجْمَ وَقَالَ لَقَدْ كُنَّا أَفْأُكًا ۖ يَوْمَ تَكُونُونَ ﴿٦١﴾

اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ لَهُ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٦٢﴾

وَلَكِنْ سَأَلْتَهُمْ مَنْ نَزَّلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ مِنْ بَعْدِ مَوْتِهَا ۖ لِيَقُولَنَّ اللَّهُ ۖ قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٦٣﴾

وَمَا هَذِهِ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا لَهُوٌّ لَّعِبٌ ۚ وَإِنَّ الدَّارَ الْآخِرَةَ لَهِيَ الْحَيَوَانُ لِمَوَكِّنَّا الَّذِينَ آمَنُوا ﴿٦٤﴾

فَإِذَا رَكِبُوا فِي الْفُلِكِ دَعُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ

Mungu, na hali ya kuwa wanamtakasishia utii. Lakini Anapowafikisha salama barani, mara wanamshirikisha;

66. Wapate kutoyashukuru Tuliowapa, na wapate kustarehe (kwa yale mabaya yao). Lakini karibuni hivi watajua!

67. Je, hawaoni ya kwamba Tumeifanya (nchi yao) nchi takatifu na ya amani, hali ya kuwa wanabwakuliwa watu wa pembezoni mwao? Je, wanaamini batili na kuzikufuru neema za Mwenyezi Mungu?

68. Na nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzushia uwongo Mwenyezi Mungu, au anayekadhibisha haki inapomjia? Je, si katika Jahanamu yatakuwa makazi ya makafiri?

69. Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia Zetu. Na bila shaka Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wafanyao mema.


الَّذِينَ هُمْ يَكْفُرُونَ إِلَى اللَّهِ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ ١٥

لِيَكْفُرُوا بِمَا آتَيْنَاهُمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ١٦

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا جَعَلْنَا حَرَمًا مَّا أُمْنَا فَتَنَ الْكَافِرِينَ ١٧
مِنْ حَوْلِهِمْ أَفِيَالٌ بَاطِلٌ يُؤْمِنُونَ وَبِنِعْمَةِ اللَّهِ
يَكْفُرُونَ ١٨

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا
أَوْ كَذَّبَ بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُ أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ
مَثْوًى لِّلْكَافِرِينَ ١٩

وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِينَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا
وَإِنَّ اللَّهَ لَمَعَ الْمُحْسِنِينَ ٢٠



SURATUR RUM

(Imeteremka Makka)

Ina Aya 60

Ina Makara 6

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Alif Lam Mym.

الْم

2. Warumi wameshindwa

غُلِبَتِ الرُّومُ

3. Katika nchi iliyo karibu (na nchi ya Bara Arabu. Nayo ni Shamu); nao baada ya kushindwa kwao, watashinda

فِي أَدْنَى الْأَرْضِ وَهُمْ مِنْ بَعْدِ عَلَيْهِمْ
سَيِّقِيُونَ

4. Katika myaka michache; Amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla (yake) na baada (yake); na siku hiyo Waislamu watafurahi

فِي بَضْعِ سِنِينَ ۚ لِلَّهِ الْأَمْرُ مِنْ قَبْلُ وَمِنْ
بَعْدُ ۚ وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ

5. Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu (atakawapa wao. Nayo ni kuwashinda Makureshi siku hiyo). (Mwenyezi Mungu) humnusu Amtakaye; naye ni Mwenye nguvu (na) Mwenye rehema.

يَنْصُرُ اللَّهُ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ ۚ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ

6. (Hii ni) ahadi ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu Havunji ahadi yake, lakini watu wengi hawajui.

وَعَدَ اللَّهُ لَا يَخْلِفُ اللَّهُ وَعْدَهُ وَلَكِنْ أَكْثَرُ
النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

7. Wanajua hali ya dhahiri ya maisha ya dunia, na wameghafilika na akhera.

يَعْلَمُونَ ظَاهِرًا مِّنَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَهُمْ
عَنِ الْآخِرَةِ هُمْ غَفْلُونَ

8. Je, hawafikiri katika nafsi zao (wakaona kuwa): Mwenyezi Mungu Hakuumba mbingu na

أَوَلَمْ يَتَفَكَّرُوا فِي أَنفُسِهِمْ مَّا خَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ

2. Sura hii imepata jina katika bishara inayoeleza kuwa Warumi watawashinda. Waajemi ambao wakati ilipotolewa bishara hii wao. Warumi walikuwa wameshindwa kabisa na milki zao zimekwishaingia mikononi mwa Waajemi. Sura hii inajulikana kuwa ya Makka na ilishuka katika mwaka wa sita au wa saba kabla ya Hijra. (Warumi ni watu wa zamani waliotawala milki kubwa. Mji wao mkubwa ukiitwaa Rumi (Rome) nao uko katika nchi ya Italia).

Kulikuwa ugomvi baina ya falme mbili — Rumi na Ajemi — ulioanza katika mwaka 602 A.D. Na katika mapigano hayo, Waajemi waliwashinda Warumi. Habari za kushinda Waajemi zilipofika Makka, makafiri walifurahi sana, maana Waajemi walikuwa wakiabudu masanamu kama wao. Makafiri wakasema kuwaambia Waislamu, "Wakiristo, watu wa Kitabu kama nyinyi, nao wameshindwa na washirikina wenzetu, na hii ni alama ya kuwa karibuni na sisi tutakushindeni."

Qurani ikatangaza Aya hizi zenye bishara mbili: Bishara ya kwanza ni kuwa katika muda wa kiasi cha miaka tisa Waajemi watashindwa na ya pili siku hiyo Waislamu watafurahi, yaani makafiri wa Makka nao watashindwa.

Katika mwaka 624 Hirakla, mfalme wa Warumi, aliingia Media (Madayin) katika nchi ya Ajemi. Na katika mwaka huu huu Waislamu 313 walilishinda jeshi la makafiri 1,000 mastadi wa vita waliokuja kwa nia ya kuwaangamiza. Vita vikapiganwa katika mtaa wa Badri na makafiri wakashindwa vibaya. Kwa hivyo bishara iliyotangazwa hapa ikatimia.

ardhi na vilivyomo ndani yake ila kwa haki na kwa muda uliowekwa? Na kwa yakini watu wengi hawakubali ya kwamba watakutana na Mola wao.

9. Je, hawatembai katika nchi na kuona jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? Nao walikuwa wenye nguvu zaidi kuliko wao, na wakilima ardhi na kuistawisha zaidi kuliko wao walivyoistawisha, na Mitume wao waliwajia kwa dalili waziwazi, basi hakuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwadhulumu, lakini walikuwa wenyewe wakijidhulumu nafsi zao.

10. Kisha ulikuwa mwisho wa wale waliofanya ubaya ni kuzikadhibisha Aya za Mwenyezi Mungu, na walikuwa wakizicheza shere (kuzifanyia mzaha).

11. Mwenyezi Mungu Ameanzisha viumbe, tena atavirudisha (mara ya pili) kisha mtarudishwa Kwake.

12. Na siku kitakaposimama Kiama waovu watakata tamaa (ya kupata rehema za Mwenyezi Mungu).

13. (Wala) hawatakuwa na waombezi miongoni mwa waliokuwa wakiwashirikisha, na washirikishwa hao watawakataa.

14. Na siku kitakapotokea Kiama, siku hiyo watafarikiana (viumbe; hawa wende Peponi na hawa wende Motoni).

15. Wale walioamini na kutenda mema watafurahishwa katika bustani.

16. Na wale waliokufuru na wakazikadhibisha Aya Zetu na makutano ya akhera, hao watahudhurishwa katika adhabu (ya Moto).

17. Basi Mtukuzeni Mwenyezi Mungu mnapoingia katika nyakati za usiku (kwa kusali Magharibi na Isha) na mnapoingia katika asubuhi (kwa kusali sala ya Alfajiri).

18. Na sifa zote njema ni Zake Mwenyezi Mungu mbinguni na ardhi. Na (mtukuzeni) wakati wa Alasiri na mnapoingia katika wakati wa Adhuhuri.

19. Hukitoa kilicho hai katika kilichokufa, na Hukitoa kilichokufa katika kilicho hai, na huihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Na hivyo ndivyo mtakavyofufuliwa.

وَالْأَرْضُ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ وَأَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ بِلِقَائِي رَبِّهِمْ لَكٰفِرُونَ ①
أَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۚ كَانُوا أَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً وَأَثَارُوا الْأَرْضَ وَعَمَرُوهَا أَكْثَرَ مِمَّا عَمَرُوهَا وَجَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ ۖ فَمَا كَانَ اللَّهُ لِيَظْلِمَهُمْ وَلٰكِن كَانُوا أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ②

لَّمْ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ آسَاءَ وَالسَّوَاءِ أَنْ كَذَّبُوا بِآيَاتِ اللَّهِ وَكَانُوا بِهَا يَسْتَهْزِئُونَ ③
اللَّهُ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ④

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُبْلِسُ الْمُجْرِمُونَ ⑤

وَلَمْ يَكُنْ لَهُم مِّنْ شُرَكَائِهِمْ شُفَعَاءُ وَكَانُوا بِشُرَكَائِهِمْ كَافِرِينَ ⑥
وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُنْفِقُونَ ⑦

فَأَمَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَهُمْ فِي رَوْضَةٍ يُحْبَرُونَ ⑧

وَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَلِقَائِ الْآخِرَةِ فَأُولَٰئِكَ فِي الْعَذَابِ مُحْضَرُونَ ⑨
فَسَبِّحْ لِلَّهِ حِينَ تُمْسُونَ وَحِينَ تُصْبِحُونَ ⑩

وَلَهُ الْحَمْدُ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَعَشِيًّا وَحِينَ تُظْهِرُونَ ⑪

يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَيُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ وَكَذَٰلِكَ تُخْرَجُونَ ⑫

20. Na katika Ishara zake (za kuonyesha uweza wake) ni huku kukuumbeni kwa udongo, kisha mumekuwa watu mnaoenea (kila mahali).

21. Na katika Ishara Zake (za kuonyesha ihsani zake juu yenu) ni kuwa Amekuumbieni wake zenu katika jinsi yenu ili mupate utulivu kwao, naye Amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Bila shaka katika haya zimo Ishara kwa watu wanaofikiri.

22. Na katika Ishara Zake (za kuonyesha uweza wake) ni kuumba mbingu na ardhi, na kuhitalifiana lugha zenu na rangi zenu na (mengine yenu, na hali ya kuwa Muumbaji ndiye huyo huyo mmoja). Kwa yakini katika haya zimo Ishara kwa wenye ujuzi.

23. Na katika Ishara Zake (za kuonyesha hikima yake) ni kulala kwenu usiku na (kuamka) mchana, na kutafuta kwenu fadhila Yake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaosikia.

24. Na katika Ishara Zake (za kuonyesha nguvu zake) ni kukuonyesheni umeme kwa (kukutieni) hofu na tamaa (ya kuja mvua), na kuyateremsha (hayo) maji kutoka mawinguni, kwayo Huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Bila shaka katika haya zimo Ishara kwa watu wanaofahamu.

25. Na katika Ishara zake (za kuonyesha uweza wake) ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa amri Yake; kisha Atakapokuiteni wito mmoja tu, (nyote) mtatoka ardhini.

26. (Vyote) vilivyo mbinguni na ardhini ni Vyake, na vyote humtii yeye.

27. Na Yeye ndiye Aliyeanzisha viumbe na ndiye Atakayevirudisha (mara nyingine), na (jambo) hili ni rahisi zaidi Kwake; naye ndiye mwenye sifa nzuri mbinguni na katika ardhi, naye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

28. Amekupigieni mfano kwa hali ya nafsi zenu; je, katika hao iliyowatamalaki mikono yenu ya kuume, (kulia) muna washirika katika yale Tuli yokupeni, hata mnashirikiana sawa sawa, mnawaogopa kama mnavyoogopana wenyewe? (Mbona nyinyi mnafanya Mwenyezi Mungu ana washirika katika waja wake?) Namna hivi tunazipambanua Aya (zetu) kwa watu wanaofahamu.

29. Lakini waliodhulumu (nafsi zao) wamefuata matamanio yao pasipo kujua; basi ni nani awezaye kumuongoza ambaye Mwenyezi Mungu Amemuacha

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ إِذَا أَنْتُمْ بَشَرٌ تَنْتَشِرُونَ ﴿٢٠﴾

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٢١﴾

وَمِنْ آيَاتِهِ خَلْقُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَخِلَافٌ أَلَيْسَ لَكُمْ أَنْتُمْ وَآلَاؤُكُمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِلْعَالَمِينَ ﴿٢٢﴾

وَمِنْ آيَاتِهِ مَنَامُكُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَابْتِغَاءُكُمْ مِنَ فَضْلِهِ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يُسْمِعُونَ ﴿٢٣﴾

وَمِنْ آيَاتِهِ يُرِيكُمْ الْبَرْقَ خَوْفًا وَطَمَعًا وَيُنَزِّلُ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَيُخْرِجُ بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٢٤﴾

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ تَقُومَ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ بِأَمْرِهِ ثُمَّ إِذَا دَعَاكُمْ دَعْوَةً مِنْ الْأَرْضِ إِذَا أَنْتُمْ تَخْرُجُونَ ﴿٢٥﴾

وَلَهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ كُلُّ لَهُ قَنَتُونَ ﴿٢٦﴾

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ وَلَهُ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢٧﴾

ضَرَبَ لَكُمْ مَثَلًا مِنْ أَنْفُسِكُمْ ۖ هَلْ لَكُمْ مِنْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِنْ شُرَكَاءَ فِي مَا رَزَقْتَكُمْ فَأَنْتُمْ فِيهِ سَوَاءٌ ۚ لَكُمْ فَوَنُفُوسُكُمْ أَحْيَاكُمْ أَنْفُسَكُمْ ۖ كَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٢٨﴾

بَلِ اتَّبَعَ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَهْوَاءَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۚ فَمَنْ

kupotea (kwa kuwa mwenyewe hataki kuongoka)?
Nao hawatakuwa na wenye kuwanusuru.

30. Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo sawasawa — ndilo umbile Mwenyezi Mungu Alilowaambia watu; (yaani dini hii ya Kiislamu inawafikiana barabara na umbo la binadamu). Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini iliyo haki, lakini watu wengi hawajui.

31. Nyenyekeeni Kwake na Mcheni, na simamisheni Sala, wala msiwe katika washirikina

32. Katika wale walioitenga dini yao na wakawa makundi makundi; kila kikundi kinafurahia kilicho nacho.

33. Yakiwapata watu madhara humuomba Mola wao kwa kumnyenyekea, kisha Anapowaonjesha rehema Yake, hapo baadhi yao mara humshirikisha Mola wao

34. Kwa kuyakanusha Tuliowapa; basi stareheni (kwa hayo Mnayoyapenda); karibuni hivi mtajua (ubaya wake).

35. Je, Tumewateremshia dalili inayowatolea hoja kwa huo ushirikina wao?

36. Na tunapowaonjesha watu rehema, huifurahia, na kama ukiwafika ubaya kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yao, mara wanakata tamaa.

37. Je, hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu (Hutoa), humkunjulia riziki nyingi amtakaye na Hudhikisha (kwa amtakaye)? Bila shaka katika haya zimo Ishara kwa watu wanaoamini.

38. Basi mpe jamaa haki yake na masikini na msafiri (aliyecharibikiwa). Hayo ni bora kwa wale wanaotaka radhi ya Mwenyezi Mungu; na hao ndio watakaofuzu.

39. Na zile (pesa za kukopeshea) riba mtoazo (katika kuwakopesha watu) ili zizidi katika mali ya watu, mbele ya Mwenyezi Mungu hazizidi (pesa hizo; bali zinaingia nuhusi na shakawa); lakini (mali)

يَهْدِي مَنْ أَضَلَّ اللَّهُ، وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ ۝
فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا، فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي
فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا، لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ
ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ ۚ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا
يَعْلَمُونَ ۝

مُنِيبِينَ إِلَيْهِ، وَاتَّقُوا وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَلَا تَكُونُوا
مِنَ الْمُشْرِكِينَ ۝

مِنَ الَّذِينَ فَتَحُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا تَشِيْعًا، كُلَّ حِزْبٍ
بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُوا ۝

وَإِذَا مَسَّ النَّاسَ ضُرٌّ دَعَوْا رَبَّهُمْ مُنِيبِينَ إِلَيْهِ
ثُمَّ إِذَا أَذَاهُمْ مِّنْهُ رَحِمَهُ إِذَا فَرِيقٌ مِّنْهُمْ بِرَبِّهِمْ
يُشْرِكُونَ ۝

لِيَكْفُرُوا بِمَا آتَيْنَهُمْ، فَتَمُوتُوا فَسَوْفَ
تَعْلَمُونَ ۝

أَمْ أُنزِلْنَا عَلَيْهِمْ سُلْطَانًا فَهُوَ يَتَكَلَّمُ بِمَا كَانُوا بِهِ
يُشْرِكُونَ ۝

وَإِذَا أَذَقْنَا النَّاسَ رَحْمَةً فَرِحُوا بِهَا، وَإِنْ تُضِلُّهُمْ
سَبِيلَةً، يَمَّا قَدَّمَتْ أَيْدِيَهُمْ إِذَا هُمْ يَقْنَطُونَ ۝
أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ
إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ۝

قَاتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ
ذَٰلِكَ خَيْرٌ لِّلَّذِينَ يُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ وَأُولَٰئِكَ
هُمْ الْمُقْلِحُونَ ۝

وَمَا آتَيْتُم مِّن رِّبَا لِّيَرْبُوَا فِي أَمْوَالِ النَّاسِ فَلَا
يَرْبُوا عِنْدَ اللَّهِ، وَمَا آتَيْتُم مِّن زَكَاةٍ تُرِيدُونَ

38. Aya hii ndiyo dalili ya wanavyuoni wasemao kwamba mwenye nafasi ni Wajibu kuwasaidia wasiokuwa na nafasi, katika jamaa zake na wengineo. Wala haki hii si katika Zaka ni katika Sadaka.

39. Riba ni kinyume cha Zaka. Riba dhahiri yake ni kupata zaidi, lakini huleta ukorofi. Na Zaka, dhahiri yake ni kupungukiwa, lakini huleta baraka. Mungu ametoa ahadi ya kumpiga vita mlaji riba (2:279).

mnayoyatoa kwa ajili ya Zaka kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi hao (wenye kufanya haya) ndio wazidishao (mali zao).

40. Mwenyezi Mungu ndiye Aliyekuumbeni, kisha Akakupeni riziki, kisha Atakufisheni, kisha Atakufufueni. Je, miongoni mwa wale mnaowashirikisha na Mungu yuko awezaye kufanya lolote katika haya? Yeye (Mwenyezi Mungu) ameepekana na upungufu, na ameepekana na wale wanaomshirikisha (naye).

41. Uharibifu umedhihiri barani na baharini kwa sababu ya yale iliyoyafanya mikono ya watu, ili Awaonjeshe (adhabu ya) baadhi ya mambo waliyoyafanya, hwenda wakarudi (wakatubia kwa Mwenyezi Mungu).

42. Sema: "Safirini katika ardhi na tazameni jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale waliotangulia. Wengi wao walikuwa ni wenye kushirikisha."

43. Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo ya haki kabla ya kufika hiyo siku isiyozuilika, inayotoka kwa Mwenyezi Mungu, siku hiyo watatengana (watu — wazuri wende Peponi na wabaya wende Motoni).

44. Anayekufuru, (madhara ya) kufuru yake ni juu yake (mwenyewe); na wafanyao mema, (hao) wanazitengenezea nafsi zao

45. Ili Awalipe wale walioamini na kufanya vitendo vizuri katika fadhila Zake. Bila shaka Yeye Hawapendi makafiri.

46. Na katika Ishara Zake (za kuonyesha rehema yake) ni kuzileta pepo ziletazo habari nzuri (ya kuwa mvua inakuja), na ili kuwaonjesheni rehema Yake, na ili vyende vyombo (baharini) kwa amri Yake, na mzitafute fadhila Zake, na ili mumshukuru.

47. Na kwa hakika Tuliwatuma kabla yako Mitume kwa watu wao, na wakawajia kwa hoja waziwazi. Kisha Tukawaadhibu wale waliofanya mabaya; na ni wajibu juu Yetu kuwanusuru wanaoamini.

41. Haya yanayotufika — mengi katika hayo — ni kwa mabaya yetu wenyewe. Tumeyataka wenyewe, wache yatutotore. Kwa ugonjwa wa kujitakia mtu haambiwi "pole." Ataambiwa "Astaili yako." Basi natuurejeele mwendo wetu mzuri, yatarejea yetu mazuri, kama alivyotwambia Mwenyewe Mwenyezi Mungu mara nyingi; kama katika Aya ya 53 ya *Suratul Anfal* na Aya ya 11 ya *Suratur Raad* na Aya ya 7 ya *Surat Ibrahimu* na nyinginezo.

وَجَّهَ اللَّهُ قَاوَلِيكَ هُمْ الْمُضْعِفُونَ ④

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُمْ ثُمَّ رَزَقَكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ هَلْ مِنْ شُرَكَائِكُمْ مَنْ يَفْعَلُ مِنْ ذَلِكَ مِمَّنْ شَيْءٌ سُبْحَنَهُ وَتَعَالَى عَمَّا يُشْرِكُونَ ⑤

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُذِيقَهُمْ بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ⑥

قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلُ كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُشْرِكِينَ ⑦
فَاقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ الْقَيِّمِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا مَرَدٍّ لَهُ مِنَ اللَّهِ يَوْمَئِذٍ يُصَدِّعُونَ ⑧

مَنْ كَفَرَ فَعَلَيْهِ كُفْرُهُ وَمَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلَا نَفْسَ لَهُمْ يَهْدُونَهُ ⑨

لِيَجْزِيَ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْ فَضْلِهِ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْكَافِرِينَ ⑩

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ يُرْسِلَ الرِّيَّاحَ مُبَشِّرَاتٍ وَلِيُذِيقَكُمْ مِنْ رَحْمَتِهِ وَلِتَجْرِيَ الْفُلُكُ بِأَمْرِهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ وَلِعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ⑪

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ رُسُلًا إِلَى قَوْمِهِمْ فَجَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَانْتَقَمْنَا مِنَ الَّذِينَ أَجْرُمُوا وَكَانَ حَقًّا عَلَيْنَا نَصْرُ الْمُؤْمِنِينَ ⑫

48. Mwenyezi Mungu ndiye Anayezileta pepo zikaharikisha mawingu, kisha Akayatandaza (hayo mawingu) mbinguni kama Apendavyo, na Akayafanya mapande mapande, kisha unaona mvua ikinyesha ndani yake; na Anapoifikisha kwa awatakao katika waja wake, mara utawaona wamefurahi.

49. Na ingawa kabla ya kuteremshiwa walikuwa wenye kukata tamaa.

50. Basi ziangalie alama za rehema ya Mwenyezi Mungu, jinsi Anavyoihuisha ardhi baada ya kufa kwake; bila shaka Yeye ndiye Mwenye kuhuisha wafu, naye ndiye Mwenye uweza juu ya kila kitu.

51. Na kama Tukileta upepo na wakauona umekuwa rangi ya manjano (kwa ghadhabu zake); juu ya haya wangeendelea kukufuru.

52. Na wewe, bila shaka, huwezi kuwasikilizisha wito wako wafu, wala huwezi kuwasikilizisha viziwi, watakapogeuka wanakwenda zao.

53. Wala huwezi kuwaongoa vipofu katika upotofu (upotevu) wao. Huwasikilizishi ila wanaoziamini Aya Zetu; hao ndio wenye kunyenyekea.

54. Mwenyezi Mungu ndiye Aliyekuumbeni katika udhaifu, na baada ya udhaifu Akafanya nguvu, kisha baada ya nguvu Akaufanya udhaifu na uzee. Anaumba appendavyo; naye ni Mjuzi, Mwenye uweza.

55. Na siku kitakaposimama Kiama waovu wataapa (ya kwamba) hawakukaa (ulimwenguni) isipokuwa saa moja tu, (kwa kishindo watachokiona). Na namna hivi ndivyo walivyokuwa wakipotolewa (walivyokuwa wakigeuzwa na haki).

56. Na waliopewa ilimu na imani watasema: "Hakika nyinyi mumekaa kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu mpaka siku ya kufufuliwa, basi hii ni siku ya kufufuliwa, lakini nyinyi mlikuwa hamjui."

57. Siku hiyo haitawafaa waliodhulumu udhuru wao, wala haitapokelewa toba yao.

اللَّهُ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيَّحَ تَنْشِيرًا سَابًا فَيَبْسُطُهُ فِي السَّمَاءِ كَيْفَ يَشَاءُ وَيَجْعَلُهُ كِسْفًا فَتَرَى الْوَدْقَ يَخْرُجُ مِنْ خِلَالِهِ، فَإِذَا أَصَابَ بِهِ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادَةٍ إِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٥٨﴾

وَلَنْ كَانُوا مِنْ قَبْلِ أَنْ يُنْزَلَ عَلَيْهِمْ مِنَ قَبْلِهِ لُمْلِسِينَ ﴿٥٩﴾

فَإِنْظِرْ إِلَى أَنْزَلْنَاهُ اللَّهُ كَيْفَ يُعْجِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا إِنَّ ذَلِكَ لَمِنْ عَجَائِ الْمَوْتَى، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٦٠﴾

وَلَنْ أَرْسَلْنَا رِجَالًا قَرِيبًا فَرَؤُهُ مُصْغَرًا لَظُلُومًا مِنْ بَعْدِهِ يَكْفُرُونَ ﴿٦١﴾

فَأَنْتَ لَا تَعْلَمُ الْمَوْتَى وَلَا نَسِئَهُ الصُّمِّ الدُّعَاءُ إِذَا وَلَّوْا مُدْبِرِينَ ﴿٦٢﴾

وَمَا أَنْتَ بِهَادٍ الْعَمَى عَنْ صَلَاتِهِمْ، إِنَّ تَنْصِرُ إِلَّا مَنْ يُؤْمِنُ يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ فَهُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٦٣﴾

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ ضَعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ ضَعْفٍ قُوَّةً ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ قُوَّةٍ ضَعْفًا وَشَيْبَةً، يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ، وَهُوَ الْعَلِيمُ الْقَدِيرُ ﴿٦٤﴾

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُقْسِمُ الْمُجْرِمُونَ مَا لَبِثُوا غَيْرَ سَاعَةٍ كَذَلِكَ كَانُوا يُؤْفَكُونَ ﴿٦٥﴾

وَقَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ وَالْإِيمَانَ لَقَدْ لَبِثْنَا فِي كِتَابِ اللَّهِ إِلَى يَوْمِ الْبَعْثِ، فَهَذَا يَوْمُ الْبَعْثِ وَلَكِنَّكُمْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٦﴾

فَيَوْمَئِذٍ لَا يَنْفَعُ الَّذِينَ ظَلَمُوا مَعْدِرَتُهُمْ وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٦٧﴾

48. Namna hivi Mwenyezi Mungu anataja kufanyika mawingu mpaka ikanyesha mvua, kama wanavyosema sasa wenye ilimu ya *Geography* na mengineyo. Basi mvua inafanyika papa hapa katika MAWINGU, siyo inatoka katika MBINGU, kama vinavyosema vitabu vyingine bila ya kufuata maneno ya Mwenyezi Mungu.

Basi hili vile vile ni katika hayo yaliyosemwa katika Aya ya 42 ya *Surat Haa Mym Sajdah*: kuwa Haliwezi kuwa uwongo lililosemwa katika Qurani.

58. Na kwa yakini Tumepiga mfano wa kila namna kwa ajili ya watu katika Qurani hii. Na kama ukiwajia na hoja yoyote ile, bila shaka wale waliokufuru watasema: "Hamkuwa nyinyi ila ni wabatilishaji (haki)."


59. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyopiga muhuri katika nyoyo za wale wasiofahamu.

60. Basi subiri, bila shaka ahadi ya Mwenyezi Mungu ni haki, wala wasikupaparishe wale wasio kuwa na yakini.

وَلَقَدْ ضَرَبْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا الْقُرْآنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ
وَلَكِنْ جَاءَتْهُمْ بَايَةٌ لِيَقُولُوا الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ
أَنُتِمُّوا إِلَّا مُبْطَلُونَ ﴿٥٨﴾

كَذَلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٩﴾

فَاصْبِرْ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَلَا يَسْتَخِفُّكَ الَّذِينَ
لَا يُوقِنُونَ ﴿٦٠﴾



Ina Aya 34

SURATU LUQMAN

Ina Makara 4

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Alif Lam Mym.

الْعَلَّامِ

2. Hizi ni aya za Kitabu Kilichotengenezwa vizuri kabisa

تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ الْحَكِيمِ

3. Uwongofu na rehema kwa wafanyao wema

هُدًى وَ رَحْمَةً لِّلْمُحْسِنِينَ

4. Wale wanaosimamisha Sala na kutoa Zaka, ambao wana yakini na akhera.

الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ

5. Hao ndio walio juu ya uwongofu utokao kwa Mola wao, na hao ndio wenye kufaulu, (kufuzu).

أُولَئِكَ عَلَى هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

6. Na katika watu wako wanaokhitari maneno ya upuzi ili wawapoteze watu na njia ya Mwenyezi Mungu, pasipo wao kujua lolote, na wanaicheza shere hiyo njia ya Mwenyezi Mungu. Basi hao watapata adhabu ifedheheshayo.

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَشْتَرِ لَهْوَ الْحَدِيثِ لِيُضِلَّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَيَتَّخِذَهَا هُزُوًا أُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ مُّهِينٌ

7. Na wanaposomewa Aya Zetu, huzipa mgongo kwa kujivuna kama kwamba hawakuzisikia, kama kwamba masikioni mwao mna uzito (uziwi), basi wape habari ya adhabu iumizayo.

وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِ آيَاتُنَا وَلَّى مُّسْتَكْبِرًا كَأَن لَّمْ يَسْمَعْهَا كَأَن فِيّ أذْنَهُ وَقْرًا فَنَسْفَعْهُ بِعَذَابٍ آَلِيمٍ

8. Bila shaka wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri, zitakuwa kwao mabustani ya neema (Peponi).

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ جَنَّاتُ النَّعِيمِ

9. Watakaa humo milele — ni ahaqi ya Mwenyezi Mungu iliyo haki, na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

خَالِدِينَ فِيهَا وَعَدَ اللَّهُ حَقًّا وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

10. Ameziumba mbingu pasipo nguzo, (mihimili) mزيونazo, na Ameiweka milima katika ardhi ili (ardhi) isikusukenisukeni; naye Ametawanya humo nyama wa kila namna, na Tumeysteremsha maji kutoka mawinguni, na humo Tumeotesha (mimea) mizuri ya kila aina.

خَلَقَ السَّمَوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا وَآلَتْ فِي الْأَرْضِ رَوَاسِيَ أَن تَمِيدَ بِكُمْ وَبَثَّ فِيهَا مِن كُلِّ دَابَّةٍ وَأَنزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَنبَتْنَا فِيهَا مِن كُلِّ زَوْجٍ كَرِيمٍ

11. Vyote hivi ameviumba Mwenyezi Mungu. Basi Nionyesheni ni nini walichoumba wale wasiokuwa yeye. Lakini madhalimu wa nafsi zao warno tu katika upotofu (upotevu) uliyo dhahiri.

12. Na kwa yakini Tulimpa Luqmani hikima, tukamwambia Mshukuru Mwenyezi Mungu; na atakayeshukuru, kwa yakini anashukuru kwa ajili ya nafsi yake; na atakayekufuru, Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Asifiwaye, (hahitaji kushukuriwa na yeye).

13. Na (wakumbushe), Luqmani alipomwambia Mwanawe; na hali ya kuwa anampa nasiha. Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu, maana shirki ndiyo dhuluma kubwa.

14. Na tumemuusia mwanadamu (kuwafanyia ihsani) wazazi wake — mama yake ameichukuwa mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na (kumnyonyesha na kuja) kumwachisha kunyonya katika miaka miwili — ya kwamba unishukuru Mimi na wazazi wako; marejeo yenu ni Kwangu.

15. Na (wazazi wako) wakikushurutisha kunishirikisha na (yale) ambayo huna ilimu nayo, usiwatii; lakini kaa nao kwa wema hapa duniani (maadamu ni wazee wako, ila usiwafuate tu mwendo wao mbaya); shika njia ya wale wanaoelekea Kwangu, kisha marejeo yenu ni Kwangu, hapo Nitakuambieni mliyokuwa mkiyatenda.

16. Ewe mwanangu! Kwa hakika jambo lolote lijapokuwa na uzito wa chembe ya hardali, likawa ndani ya jabali au mbinguni au katika ardhi, Mwenyezi Mungu Atalileta (amlipe aliyefanya); bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo yaliyofichikana, (na) Mjuzi wa mambo yaliyo dhahiri.

17. Ewe mwanangu! Simamisha Sala, na uamrishe mema, na ukataze mabaya, na usubiri juu

هَذَا خَلَقَ اللَّهُ قَارُونَ مَاذَا خَلَقَ الَّذِينَ مِنْ دُونِهِ ۚ بَلِ الظَّالِمُونَ فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ۝

وَلَقَدْ آتَيْنَا لُقْمَانَ الْحِكْمَةَ أَنْ اشْكُرْ لِلَّهِ وَمَنْ يَشْكُرْ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ حَبِيدٌ ۝

وَإِذْ قَالَ لُقْمَانُ لِابْنِهِ وَهُوَ يُعْظَمُ يَا بُنَيَّ لَا تُشْرِكْ بِاللَّهِ إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ۝

وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا ۖ وَالْهَنَاءُ عَلَى وَهْنٍ ۖ وَفَضْلُهُ فِي غَمٍّ ۖ إِنَّ الشُّكْرَ لِي ۖ وَلِوَالِدَيْكَ إِلَى الْمَصِيرِ ۝

وَإِنْ جَاهَدَكَ عَلَى أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا ۚ وَصَاحِبُمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا ۚ وَآتِ بِسَبِيلٍ مِّنْ أَمَّا إِلَيَّ ثُمَّ إِلَىٰ مَرْجِعِكُمْ فَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ۝

يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكَ فِي تِلْكَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ ۚ فَتَكُنْ فِي صَخْرَةٍ أَوْ فِي السَّمَوَاتِ أَوْ فِي الْأَرْضِ يَأْتِ بِهَا اللَّهُ ۚ إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ۝

يُبَيِّنُ آفِيمَ الصَّلَاةِ وَأَمْرَ بِالْمَعْرُوفِ وَانْهَ عَنِ

11. Inataka wasikie vizuri haya hao wanaoyaomba makaburi na mizimu na . . . iwape mtoto, na kama haya. Tangu lini hao wamekuwa waumbaji? Hebu nawatuonyeshe hivyo walivyoumba. Hawawachi watu! Wanataka waambiweje zaidi kuliko hivi?

13. Amekuumba Mwenyezi Mungu, unamuabudu mwengine!

Huyu Luqmani ni katika mabwana wakubwa wema kabisa waliokuwako ulimwenguni. Lakini Mwenyezi Mungu hakutwambia — wala haikusini katika Hadithi ya Mtume — kuwa alikuwa wa Kabila gani wala Mahala gani wala Wakati gani. Wala si muhimu kuyajua haya. Muhimu kuyajua mwendo wake tukaufuata. Nao ndio huu aliotuajia Mwenyezi Mungu hapa katika Aya ya 13 na ya 16 na ya 17 na ya 18 na ya 19.

15. Katika maelezo ya Aya waliyofanya ni ya 16 wametia ukafiri wao wa kumtaja mtu wao na kitabu chake cha kupoteza.

16. Udogo wa Khardali ni kama maweale.

17. Ukiamrisha mema au kukataza mabaya lazima itakufika misukosuko. Basi usione hiyo ni misukosuko ya

ya yale yatayokusibu (kwani mwenye kuamrisha mema na kukataza mabaya lazima zitamfika tu taabu); Hakika hayo ni katika mambo yanayostahiki kuazimiwa (na kila mtu).

18. Wala usiwatazame (usiwafanyie watu jeuri), kwa upande mmoja wa uso, wala usende katika nchi kwa maringo; hakika Mwenyezi Mungu Hampendi kila ajivunae, ajifahirishaye.

19. Na ushike mwendo wa katikati, na uteremshe sauti yako; bila shaka sauti ya punda ni mbaya kuliko sauti zote (kwa makelele yake ya bure).

20. Je! Hamuoni ya kwamba Mwenyezi Mungu amekutiishieni vilivyomo mbinguni na ardhini, na Akakukamilishieni neema Zake zilizo dhahiri na za siri? Na wako watu wanaobishana katika (mambo ya) Mwenyezi Mungu pasipo ilimu wala uwongofu wala Kitabu chenye nuru.

21. Na wanapoambiwa, "Fuateni Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu," husema: "Bali tunafuata tuliyowakuta nayo baba zetu." Je!, ijapokuwa shetani anawaita katika adhabu ya Moto (uwakao)? (Watauwendea tu maadamu wazee wao waliuwendea?)

22. Na ajisalimishaye uso wake kwa Mwenyezi Mungu, na hali ya kuwa anawafanyia mema (viumbe wenziwe), bila shaka amekwishakamata fundo lililo madhubuti; na mwisho wa mambo yote ni kwa Mwenyezi Mungu.

23. Na anayekufuru, isikuhuzunisha kufuru yake, marejeo yao ni Kwetu, hapo Tutawaambia yale waliyoyafanya; hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa (hata) yaliyomo vifuani.

24. Tutawastarehesha kidogo (hapa ulimwenguni), kisha tutawasukuma katika adhabu ngumu.

25. Na kama ukiwauliza, "Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi?" Bila shaka watasema "Mwenyezi Mungu." Basi waambie: — Shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu, (wa kuabudiwa yeye peke yake), lakini wengi katika wao hawajui (lolote).

Mwenyezi Mungu ukavunjika moyo. Ona kuwa ni misukosuko iliyokufika kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu, uone kuwa utalipwa malipo mazuri kabisa akhera. Uzidi kuendelea na kazi yako hiyo ya kheri. Hakuna kizuri kinachopatikana bure.

20. Yatazame zaidi maelezo yake katika Aya ya 13 ya Suratul Jaathiya.

22. Kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu ni kufuata Amri zake kwa furaha na uchangamfu, katika unalolipenda na usilolipenda.

النَّكَرَ وَاصْبِرْ عَلَىٰ مَا أَصَابَكَ إِنَّ ذَٰلِكَ مِنْ
عَزْمِ الْأُمُورِ ۝

وَلَا تُصَيِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَتَّبِعْ فِي الْأَرْضِ
مَرْحًا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ۝

وَأَقْصِدْ فِي مَشْيِكَ وَاعْصِصْ مِنْ صَوْتِكَ إِنَّ
كَ أَنْتَ الْأَصَوَاتِ لَصَوْتُ الْحَمِيرِ ۝

أَلَمْ تَرَوْا أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُم مَّا فِي السَّمَوَاتِ
وَمَّا فِي الْأَرْضِ وَأَسْبَغَ عَلَيْكُمْ نِعَمَهُ ظَاهِرَةً
وَبَاطِنَةً وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ
بِغَيْرِ عِلْمٍ وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُّنبِئٍ ۝

وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا بَلْ
نُتَّبِعُ مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا أَوَلَوْ كَانَ
الشَّيْطَانُ يَدْعُوهُمْ إِلَىٰ عَذَابِ السَّعِيرِ ۝

وَمَن يَسْلَمْ وَجْهَهُ إِلَى اللَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ
 فَقَدْ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ ۚ وَإِلَى اللَّهِ
عَاقِبَةُ الْأُمُورِ ۝

وَمَن كَفَرَ فَلَا يَحْزُنكَ كُفْرُهُ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ
 فَمَتِّعُهُمْ بِمَا عَمِلُوا وَإِلَى اللَّهِ عَلَيْهِمْ يَدَاتِ الصُّدُورِ ۝

مُتَّبِعُهُمْ فَبَلَاءٌ ثُمَّ نَضَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ ۝

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ
 لَيَقُولُنَّ اللَّهُ قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ بَلْ أَكْثَرُهُمْ
 لَا يَعْلَمُونَ ۝

26. Kila kilichomo mbingani na ardhini ni cha Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mkwasi, Mwenye kusifiwa.

27. Na lau kama miti yote iliyomo katika ardhi ingalikuwa kalamu, na bahari hii (ikafanywa wino), na ikasaidiwa na (kuongezewa maji) na bahari nyingine saba, maneno ya Mwenyezi Mungu ya-singalikwisha. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.

28. Hakukuwa kuumbwa kwenu wala kufufuliwa kwenu ila kama nafsi moja; (hapana taabu yoyote kwa-ke Mwenyezi Mungu); hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona.

29. Je, huoni ya kwamba Mwenyezi Mungu Huuingiza usiku katika mchana, na Huuingiza mchana katika usiku, na Amelitiisha jua na mwezi; vyote vinakwenda tu mpaka wakati uliowekwa, na Mwenyezi Mungu Anazo habari za mnayoyatenda (yote).

30. Hivi ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni haki (yuko); na wanachokiomba badala yake ni batili (hakiko), (ni uwongo tu kwani hapana hata kimoja katika hicho kinachofanya anayofanya Mwenyezi Mungu). Na Mwenyezi Mungu ndiye Mtukutu (na ndiye) Mkubwa.

31. Je, huoni kwamba vyombo hupita baharini kwa neema ya Mwenyezi Mungu, ili Akuonyesheni Ishara (za neema) Zake (juu yenu)? Hakika katika hayo zimo Ishara kwa kila (walio wema, nao ni kila) mwenye ustahmilivu (anapokuwa taabuni) na mwenye shukrani (anapokuwa katika raha).

32. Na mawimbi yanapowafunika kama mawingu, humuomba Mwenyezi Mungu kwa kumtii kweli kweli; lakini Anapowaokowa kuwaleta barani, baadhi yao hushika mwendo wa katikati (uliyo mzuri, lakini wengine wanakanusha neema za Mwenyezi Mungu); wala hapana azikanushaye neema zetu ila mdanganyifu mkuu, kafiri mkubwa.

33. Enyi watu! Mcheni Mola wenu iogopeni siku ambayo baba hatamfaa mtoto wake wala mtoto hatamfaa baba yake hata kidogo. Bila shaka ahadi ya Mwenyezi Mungu ni haki; basi yasikudanganyeni maisha ya (hii) dunia, wala asikudanganyeni yule

لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَ الْأَرْضِ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ۝

وَلَوْ أَنَّ مَا فِي الْأَرْضِ مِنْ شَجَرَةٍ أَقْلَامٌ وَالْبَحْرُ يَبْدُءُ مِنْ بَدَاةٍ سَبْعَةُ أَبْحُرٍ مَا نَفِدَتْ كَلِمَاتُ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ۝

مَا خَلَقَكُمْ وَلَا يَعْشَكُم إِلَّا كَفَّيْسٌ وَاحِدَةٌ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ۝

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يُوَلِّجُ الْبَلَّ فِي النَّهَارِ وَيُولِّجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ وَ سَخَّرَ النَّامُوسَ وَالْقَمَرَ كُلَّ يَجْرِى إِلَى أَجَلٍ مُّسَمًّى وَأَنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ۝

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ الْبَاطِلُ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ ۝

أَلَمْ تَرَ أَنَّ الْفُلُوكَ تَجْرَى فِي الْبَحْرِ يَنْصَرِفُ إِلَيْهِمْ مِنْ آيَاتِهِ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ۝

وَإِذَا غَشِيَهُمْ مَوَّجٌ كَالظُّلَلِ دَعُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ فَلَمَّا نَجَّاهُمْ إِلَى الْبَرِّ فَمِنْهُمْ مُّقْتَصِدٌ وَمَا يَجْحَدُ بِآيَاتِنَا إِلَّا كُلُّ خَتَّارٍ كَفُورٍ ۝


يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ وَاحْشَوْا يَوْمًا لَا يَجْزِي وَالِدٌ عَنْ وَلَدِهِ وَلَا مَوْلُودٌ هُوَ جَائِزٌ عَنْ وَالِدِهِ شَيْئًا إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ فَلَا

mdanganyi mkubwa, (Iblisi) katika (mambo ya) Mwenyezi Mungu.

34. Kwa hakika ujuzi wa Kiama uko kwa Mwenyezi Mungu tu; naye Huteremsha mvua (wakati atakao), na anayajua yaliyomo matumboni (mwa viumbe wa kike—kuwa watazaa au hawazai, na watazaa wanaume au wanawake au wengi au kidogo. Hakuna anayejua isipokuwa yeye tu Mwenyezi Mungu); na nafsi yoyote haijui ni nini itachuma kesho, wala nafsi haijui itafia ardhi gani. Bila shaka Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi (ndiye) Mwenye habari (ya mambo yote).

تَعْرِفُكُمْ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَلَا يَعْرِفُكُمْ إِلَّا اللَّهُ
الْقُرْآنُ ٣٤
إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُنَزِّلُ الْغَيْثَ
وَيَعْلَمُ مَا فِي الْأَرْحَامِ وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ مِمَّا
ذَاتُ كَيْسٍ عَدَاءُ وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ
تَمُوتُ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ٣٤

34. Katika Aya hii — na nyingi nyinginezo kama hii — wanahizika wale wanaowadaia watu wao kujua Ghaybu.



Inu Aya 30

SURATUS SAJDHAH

Inu Makuru 3

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Alif Lam Mym.

2. Uteremsho wa Kitabu hiki hauna shaka kuwa umetoka kwa Mola wa walimwengu.

3. Je, wanasema: “Amekitunga mwenyewe?” (Sivyo hivyo). Bali hicho ni haki itokayo kwa Mola wako ili uwaonye watu wasiojiwa na muonyaji kabla yako; huenda wakaongoka.

4. Mwenyezi Mungu ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake, katika nyakati sita (anazojijua Mwenyewe Mwenyezi Mungu); na Akatawala katika Arshi yake. Nyinyi hamuna mlinzi wala muombezi isipokuwa yeye tu, je hamufikiri?

5. Anapitisha mambo yote yaliyo baina ya mbingu na ardhi, kisha yanapanda Kwake kwa siku moja tu ambayo kipimo chake ni myaka elfu mnayotumia nyinyi katika kuhisabu kwenu.

6. Huyu ndiye Ajuaye mambo ya ghaibu na ya dhahiri, Mwenye nguvu (na) Mwenye kurehemu

7. Ambaye Ametengeneza umbo la kila kitu, na Akaanzisha umbo la mwanadamu kwa udongo.

8. Na kisha Akakifanya kizazi chake kwa mchujo wa maji yaliyo madhalilifu.

9. Kisha Akamtengeneza na Akampulizia roho Yake, na Akakupeni masikio na macho na nyoyo; ni kidogo tu shukrani yenu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْحَمْدُ

تَنْزِيلُ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِنْ رَبِّ

الْعَالَمِينَ ﴿١﴾

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ بَلْ هُوَ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ لِتُنذِرَ

قَوْمًا مِمَّا أَتَاهُمْ مِنْ نَذِيرٍ مِمَّنْ قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ

يَهْتَدُونَ ﴿٢﴾

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي

سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَى عَلَى الْعَرْشِ مَا لَكُمْ مِنْ

دُونِهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا شَفِيعٍ أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ ﴿٣﴾

يُدِيرُ الْأَمْرَ مِنَ السَّمَاءِ إِلَى الْأَرْضِ ثُمَّ يَعْرُجُ إِلَيْهِ

فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ أَلْفَ سَنَةٍ مِمَّا تَعُدُّونَ ﴿٤﴾

ذَلِكَ عَلِيمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٥﴾

الَّذِي أَحْسَنَ كُلَّ شَيْءٍ خَلَقَهُ وَبَدَأَ خَلْقَ

الْإِنْسَانِ مِنْ طِينٍ ﴿٦﴾

ثُمَّ جَعَلَ نَسْلَهُ مِنْ سُلَالَةٍ مِنْ مَاءٍ مَهِينٍ ﴿٧﴾

ثُمَّ سَوَّاهُ وَنَفَخَ فِيهِ مِنْ رُوحِهِ وَجَعَلَ لَكُمُ السَّمْعَ

وَالْأَبْصَارَ وَالْأَفْئِدَةَ قَلِيلًا مِمَّا تَشْكُرُونَ ﴿٨﴾

4. Tumesema mara nyingi kuwa muda wa Siku Sita wa kuumba mbingu na ardhi anaoutaja Mungu apaujua Mwenyewe Mwenyezi Mungu kiasi chake; kama huo muda wa Siku Nne na wa siku Mbili aliotaja katika Surat Haa Mym Sajdah katika Aya 9 na ya 10 na ya 12.

7. Kila alichokiumba Mwenyezi Mungu amekitengeneza, amekikamilishia kila lake, hakuna nukhani; hakiwezi kutilika kosa, kama alivyotwambia katika Suratul Mulk katika Aya ya 3 na ya 4.

10. Nao husema (kwa maskhara): “Je, tutakapopotea katiika ardhi, (tukageuka mchanga) ndio tutarudishwa katika umbo jipya?” (Ndio). Bali wao hawakiri kwamba watakutana na Mola wao!

11. Sema: “Atakufisheni Malaika wa mauti aliyewakilishwa kwenu, kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu.”

12. Na ungaliwaona waovu wakiinamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao, (na kusema:) “Mola wetu! Tumekwisha kuona na tumekwisha kusikia, basi turudishe, tutafanya vitendo vizuri; hakika (sasa) tumeyakinisha.” (Ungaliwaona katika hali hiyo ungeiona dhila yao).

13. Na Tungalitaka Tungempa kila mtu uwongofu wake (kwa lazima kama tulivyowapa Malaika, lakini binadamu amepewa huria ya kufanya alitakalo — lililo jema na baya), lakini imehakikika kauli iliyotoka Kwangu: Kwa yakini Nitaijaza Jahanamu kwa wote hawa; majini na watu (ambao ni wabaya).

14. “Basi ionjeni (adhabu) kwa sababu ya kusahau makutano ya siku yenu hii; na Sisi Tutakusahauni (humo Motoni), na onjeni adhabu idumuyo kwa yale mliyokuwa mkiyatenda.”

15. Hakika wanaoziamini Aya Zetu ni wale tu ambao wanapokumbushwa kwazo huanguka kusujudu na humtukuzi Mola wao kwa (kutaja) sifa Zake, nao hawatakabari.

16. Huinuka mbavu zao kutoka vitandani wakati wa usiku ili kumuabudu Mola wao kwa kuogopa Moto na kutaraji Pepo; na hutoa (Zaka na sadaka) katika yale Tuliowapa.

17. Nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho (huko Peponi): ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyafanya.

18. Je! Mwislamu kamili atakuwa sawa na yule aliye fasiki? Hawawi sawa.

13. Angetaka Mwenyezi Mungu angemuumba Binadamu kama Malaika — hawezi kufanya mabaya. Maumbile yake ni kufanya mema tu. Kwa hivi halipwi kwa mema yake hayo kwani hayaonei taabu katiika kuyafanya. Lakini Binadamu ameumbwa na uweza wa yote mawili sawa sawa; na raha yake zaidi kufanya mabaya. Ndiyo maana akifanya mema atajaziwa Pepo na kwa mabaya atajaziwa Moto.

15,16. Zinatajiwa baadhi ya sifa za watu wazuri. Basi natuziige tupate haya waliyotajiwa kuwa watayapata. Na moja katika sifa hizo ni kuamka usiku wakafanya ibada.

وَقَالُوا مَرَدًا صَدَلْنَا فِي الْأَرْضِ إِنَّا لَفِي خَلْقٍ
جَدِيدٍ ۚ بَلْ هُمْ بِلِقَائِ رَبِّهِمْ كَفِرُونَ ﴿١٠﴾

قُلْ يَتَوَفَّكُم مَّلَكُ الْمَوْتِ الَّذِي وُكِّلَ بِكُمْ
ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١١﴾

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُرْسَلُونَ تَأْكُسُوا وُجُوهَهُمْ
عِندَ رَبِّهِمْ رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا فَارْجِعْنَا
لَعَمَلٍ صَاحِحًا إِنَّا مُوقِنُونَ ﴿١٢﴾

وَلَوْ شِئْنَا لَآتَيْنَا كُلَّ نَفْسٍ هُدًى وَلَٰكِن
حَقَّ الْقَوْلُ مِنِّي لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ
وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١٣﴾

فَذُوقُوا بِمَا نَسِيتُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا: إِنَّا نَسِينَاكُمْ
وَذُوقُوا عَذَابَ الْخُلْدِ بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

إِنَّمَا يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا الَّذِينَ إِذَا ذُكِّرُوا بِهَا
خَرُّوا سُجَّدًا وَسَبَّحُوا بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَهُمْ لَا
يَسْتَكْبِرُونَ ﴿١٥﴾

تَتَجَافَىٰ فِي جُحُوبِهِمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ
خَوْفًا وَطَمَعًا وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿١٦﴾

فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مِّمَّا أُخْفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعْيُنٍ
جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾

أَفَمَن كَانَ مُؤْمِنًا كَمَن كَانَ فَاسِقًا لَّا يَسْتَوُونَ ﴿١٨﴾

19. Wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri watakuwa na Mabustani ya makazi mazuri. Ni andao lao kwa yale waliyokuwa wakiyatenda.

20. Na wale waliofanya uovu, makazi yao ni Motoni, watakapotaka kutoka humo watarudishwa mumo humo na wataambiwa: “Onjeni tu adhabu ya Moto ambayo mlikuwa mkiikadhibisha.”

21. Na kwa yakini Tutawaonjesha adhabu hafifu (kwanza hapa ulimwenguni) kabla ya adhabu kubwa (ya akhera), labda watarejea.

22. Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayekumbushwa kwa Aya za Mola wake kisha akazikataa? Hakika sisi ni wenye kuchukua kisasi kwa wale wabaya.

23. Na bila shaka Tulimpa Musa Kitabu — basi usiwe na shaka na kukutana na Mwenyezi Mungu — na Tukakifanya uwongofu kwa wana wa Israili, (Mayahudi).

24. Na tukawafanya miongoni mwao maimamu wanaoongoa kwa amri Yetu, waliposubiri; na walikuwa wakiziyakinisha Aya Zetu.

25. Hakika Mola wako ndiye Atakayehukumu baina yao siku ya Kiama katika yale waliyokuwa wakihitilafiana.

26. Je, Haijawabainikia kuwa umma ngapi Tuliziangamiza kabla yao, na wao wanapita katika maskani yao hayo? Bila shaka katika hayo zimo Ishara; je, hawasikii?

27. Je, hawaoni ya kwamba Tunayapeleka maji katika ardhi kame (kavu); kisha kwayo Tunaiotesha mimea wanayokula wanyama wao na wao wenyewe; je, hawaoni?

28. Na wanasema: “Kuhukumiwa huko (kutakakotokea akhera) kutatokea lini; ikiwa mnasema kweli?”

أَمَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ جَنَّاتُ الْمَأْوَىٰ رُزُلًا مِّمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾

وَأَمَّا الَّذِينَ فَسَقُوا فَمَأْوَاهُمُ النَّارُ كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ يَخْرُجُوا مِنْهَا أُعِيدُوا فِيهَا وَقِيلَ لَهُمْ ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّتِي كُنْتُمْ بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿٢٠﴾

وَلَنَذِيرُهُمْ مِنَ الْعَذَابِ الْأُولَىٰ

ذُوقَ الْعَذَابِ الْأَكْبَرَ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢١﴾

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ ثُمَّ أَعْرَضَ عَنْهَا ۚ إِنَّا مِنَ الْمُجْرِمِينَ مُنتَقِبُونَ ﴿٢٢﴾

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ فَلَا تَكُنْ فِي مِرْيَةٍ مِّنْ لِّقَائِهِ وَجَعَلْنَاهُ هُدًى لِّبَنِي إِسْرَءِيلَ ﴿٢٣﴾

وَجَعَلْنَا مِنْهُمْ إِمَّةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا لَمَّا صَبَرُوا ۖ وَكَانُوا بِآيَاتِنَا يُوقِنُونَ ﴿٢٤﴾

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ يَفْصِلُ بَيْنَهُم يَوْمَ الْقِيَمَةِ فَبِمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٢٥﴾

أَوَلَمْ يَهْدِ لَهُمْ كَمْ أَهْلَكْنَا مِن قَبْلِهِمْ مِّنَ الْقُرُونِ يَمْشُونَ فِي مَسْكِنِهِمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً ۖ أَفَلَا يَسْمَعُونَ ﴿٢٦﴾

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ السَّمَاءَ إِلَى الْأَرْضِ الْجُرُزِ فَنُخْرِجُ بِهِ زُرْعًا تَأْكُلُ مِنْهُ أَنْعَامُهُمْ وَأَنْفُسُهُمْ ۖ أَفَلَا يُبْصِرُونَ ﴿٢٧﴾

وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَذَا الْفَتْحُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٨﴾

21. Haya magonjwa yanayowapata maasi, kama visonono na mengineyo, ili watanabahi waache upesi kabla hayajawatopea haya maafa ya duniani, seuze ya huko Motoni.

22. Haya ndiyo tunayoyapigia kelele kila siku: kuwa wanaambiwa ya Mwenyezi Mungu na Mtumewe, wakayapuzi kwa ajili ya yao waliyowakuta nayo watu wao.

24. Ukubwa — hata wa dini — haupatikani bure ila kwa kukabili misukosuko na kwa kustahmili. “Mstahamilivu Hula Mbivu.”


Makadiyani wameizalisha hii Aya waliyofanya kuwa ya 25. Wamejaza katika maelezo yake chungu ya mambo ambayo hayakhusiani chochote na Aya hii. Wamefanya haya ili kutia ule ukafiri wao wa kumdaia Utume mtu wao. Yoyote anayeitazama Aya hii haioni imekusanya hayo ya uzushi waliyoyataja wao.

29. Sema: Siku ya Kuhukumiwa, wale waliokufuru imani yao haitawafaa (wakitaka kusilimu huko), wala hawatapewa muda wa kungoja (wasitolewe roho wakati atakapowafikia Izraili).

قُلْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ لَا يَنْفَعُ الَّذِينَ كَفَرُوا إِيمَانُهُمْ وَلَا هُمْ يُنْتَظَرُونَ ﴿٢٩﴾

30. Basi wapuzilie mbali na ngoja (upate mema uliyoahidiwa), hakika wao (pia) wanangoja (walioahidiwa).

فَاعْرِضْ عَنْهُمْ وَانْتَظِرِ إِلَيْهِمْ مُنْتَظَرُونَ ﴿٣٠﴾



Ina Aya 73

SURATUL AHZAB (Imeteremka Madina)

Ina Makara 9

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Ewe Nabii! Endelea kumcha Mwenyezi Mungu wala usiwatii makafiri na wanafiki; bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ اتَّقِ اللَّهَ وَلَا تُطِعِ الْكَافِرِينَ وَالْمُنَافِقِينَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ①

2. Na ufuate ulioletewa wahyi (uliyofunuliwa) kutoka kwa Mola wako, kwa yakini Mwenyezi Mungu Anazo habari za (yote) mnayoyatenda

وَأَتِيعَ مَا يُوحَىٰ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ②

3. Na utawakali kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu Atosha kuwa Mlinzi.

وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ③

4. Mwenyezi Mungu Hakumuekea mwanaadamu nyoyo mbili kifuani mwake, wala Hakuwafanya wake zenu — mliolinganisha migongo yao na migongo ya mama zenu — kuwa mama zenu; wala Hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa wana wenu hasa; hayo ni maneno yenu ya vinywa vyenu; na Mwenyezi Mungu Ndiye anayesema kweli, Naye huongoa njia (ya uwongofu).

مَا جَعَلَ اللَّهُ لِرَجُلٍ مِّنْ قَلْبَيْنِ فِيْ جَوْفِهِ ۖ وَمَا جَعَلَ أَرْوَاحَكُمْ إِلَّآ تُظْهِرُونَ مِنْهُنَّ أَمْهَتِكُمْ ۖ وَمَا جَعَلَ أَدْعِيَاءَكُمْ أَبْنَاءَكُمْ ۖ ذَٰلِكُمْ قَوْلُكُمْ بِأَفْوَاهِكُمْ ۖ وَاللَّهُ يَقُولُ الْحَقَّ وَهُوَ يَهْدِي السَّبِيلَ ④

5. Waiteni kwa (ubini wa) baba zao, maana huo ndio uadilifu mbele ya Mwenyezi Mungu. Na kama hamuwajui baba zao, basi ni ndugu zenu katika dini na rafiki zenu. Wala si lawama juu yenu mkikosa, lakini (kuna lawama) katika yale ziliyoyafanya nyoyo zenu kwa kusudi, na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

أَدْعَوْهُمْ لِأَبَائِهِمْ هُوَ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ ۚ فَإِنْ لَّمْ تَعْلَمُوا آبَاءَهُمْ فَإِخْوَانُكُمْ فِي الدِّينِ وَمَوَالِيكُمْ ۚ وَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ فِيمَا أَخْطَأْتُمْ بِهِ ۚ وَلَٰكِنْ مَّا تَعَمَّدَتْ قُلُوبُكُمْ ۚ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ⑤

1. Imetwa kwa jina hili kwa ajili ya hayo makundi ya makafiri yaliyokuja kumpiga Mtume, kama tulivyobainisha kidogo katika Aya ya 9.

4. Katika zama za jahiliya mtu akitaka kumuadhibu mkewe alikuwa akimwambia, "Wewe kwangu ni kama mgongo wa mama yangu." Hivi ni kumwambia, "Wewe ni haramu juu yangu." Akisha kusema hivi, mwanamke yule huwa ni haramu juu yake maisha, wala hawezi kuolewa na mume mwengine. Na talaka hii wakiita "Dhihaar." Hapa wanakatazwa ada hii mbaya. Na katika Sura Al-Mujadilah Aya 2-4 imetajwa hukumu yake na kafara yake.

Vile vile katika Aya hii na ya pili yake inakatazwa kumrianya mtoto wa kupanga kama uliyemzaa.

6. Nabii ana haki zaidi kwa Waislamu (waliomfuata) kuliko nafsi zao, (lazima wamkinge Mtume hata kwa kutoa roho zao, seuze mali). Na wakeze ni mama zao; na wenye nasaba wana haki zaidi wao kwa wao (kwa kurithiana na kuozana na yaliyo kama hayo) katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu kuliko Waislamu (wengine) na (hata wakiwa) Muhajir (waliohama kutoka Makka kuja Madina kwa ajili ya dini). Lakini kama mkifanya wema kwa marafiki zenu (si vibaya). Haya yamekwishaandikwa Kitabuni.

7. Na (wakumbushe) Tulipochukua ahadi kwa Manabii (wote) na kwako wewe, na Nuhu na Ibrahimu na Musa na Isa mwana wa Mariamu, na tulichukua kwao ahadi ngumu

8. Ili Awaulize wakweli juu ya ukweli wao, na Amewaandalia makafiri adhabu iumizayo.

9. Enyi mlioamini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu; yalipokufikieni majeshi, Tukayapelekea upepo na majeshi msiyoyaona (ya Malaika), na Mwenyezi Mungu Anayaona (yote) mnayoyafanya.

10. Walipokujieni (kukushambulieni) kutoka juu yenu na kutoka chini yenu; na macho yalipokodoka na nyoyo zikapanda kooni, nanyi mkaanza kumdhania Mwenyezi Mungu dhana mbali mbali.

11. Hapo Waislamu walitiwa mtihamu (kweli kweli) na wakatetemeshwa kwa matetemesho makali.

12. Na waliposema wanafiki na wale wenye maradhi nyoyoni mwao, "Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawakutuahidi ila udanganyifu tu."

13. Na taifa moja miongoni mwao liliposema: "Enyi wenyeji wa Yathribu (Madina)! Hamna mahali pa kukaa nyinyi, basi rudini (makwenu msiingie katika jeshi pamoja na Muhammad)." Na kundi jingine miongoni mwao likaomba ruhusa kwa

النَّبِيِّ أُولَىٰ بِالْمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنْفُسِهِمْ وَأَزْوَاجُهُ أُمَّهَاتُهُمْ وَأُولُوا الْأَرْحَامِ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ بِبَعْضٍ فِي كِتَابِ اللَّهِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُهَاجِرِينَ إِلَّا أَنْ تَفْعَلُوا إِلَىٰ أَوْلِيَائِكُمْ مَعْرُوفًا كَانَ ذَلِكَ فِي الْكِتَابِ مَسْطُورًا ⑥

وَأَدْ أَخَذْنَا مِنَ النَّبِيِّينَ مِيثَاقَهُمْ وَمِنْكَ وَمِنْ نُوحٍ وَإِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ وَأَخَذْنَا مِنْهُمْ مِيثَاقًا غَلِيظًا ⑦

لِيَشْكَلَ الصَّادِقِينَ عَنْ صِدْقِهِمْ وَأَعَدَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا أَلِيمًا ⑧

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَاءَتْكُمْ جُنُودٌ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا وَجُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا وَكَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرًا ⑨
إِذْ جَاءَ نُوحٌ مِنْ قَوْمِهِ وَمِنْ أَصْفَلٍ مِنْكُمْ وَإِذْ رَأَيْتِ الْأَبْصَارُ وَبَلَغَتِ الْقُلُوبُ الْحَنَاجِرَ وَتَظُنُّونَ بِاللَّهُ الطُّنُونَ ⑩

هَذَا لِكِ اجْتِبَاءِ الْمُؤْمِنُونَ وَزَلْزَلُوا زَلْزَالًا شَدِيدًا ⑪
وَأَذِ يَقُولُ الْمُنْفِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَخِصْنٌ مَّا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ إِلَّا غُرُورًا ⑫
وَإِذْ قَالَتْ طَائِفَةٌ مِنْهُمْ يَا أَهْلَ يَثْرِبَ لَا مُقَامَ لَكُمْ فَارْجِعُوا وَيَسْتَأْذِنُ فَرِيقٌ مِنْهُمْ النَّبِيَّ يَقُولُونَ إِنَّ

6. Aya hii inataja uharamu wa kuwao wakeze Mtume akifa, kwani wamekwishakuwa mamama wa Waislamu wote.

9. Mwenyezi Mungu anawakumbusha Waislamu nusura aliyowapa katika vita vya *Ahzaab* (makundi); na pia huitwa vita vya *Handaki* yalipotoka makundi ya Makureshi na Waarabu wengine kwenda Madina kuwashambulia Waislamu. Mtume akatoa amri ya kuchimbwa *handaki* ili wajilinde na majeshi hayo. Yalipokuja makundi ya makafiri yasiweze kuingia, yakapiga kambi nje ya mji. Wengine walijaribu kuvuka hili *handaki*; wakauliwa. Baada ya siku kidogo hivi Mwenyezi Mungu akawapelekea mvua ya mchanga na changarawe na tufani; zikang'oa mahema yao na kutawanya vyombo vyao na kuharibu silaha zao. Na Akatiya hofu na dhana mbaya baina ya Waarabu na Mayahudi, ikawa kila taifa linamdhania mwenzake kuwa ni adui. Wakavunjika nyoyo zao, wakakimbia.

Mtume kwa kusema: “Hakika nyumba zetu ni tupu, (hapana watu, tunakwenda zetu),” lakini hazikuwa tupu, hawakutaka ila kukimbia tu.

14. Na lau kama yaliingia (Majeshi ya makafiri) juu yao katika pande zote (za Madina), kisha wakaombwa kufanya vita (juu ya Waislamu) wangevifanya, na wasingelikaa humo (Madina tena) ila muda kidogo tu (hivi, kisha tungewatolea mbali).

15. Na kwa yakini walikwishafanya ahadi na Mwenyezi Mungu zamani ya kwamba hawatageuza migongo (yao wakija makafiri kushambulia); na ahadi ya Mwenyezi Mungu ni yenye kuulizwa. (Basi wataulizwa kwa nini wakatengua ahadi).

16. Sema: “Kukimbia hakutakufaeni kama mkikimbia mauti au kuuawa, na kwa hivyo, (kwa kukimbia kwenu huku) hamtastareheshwa ila kidogo tu, (kisha mara mtakufa).”

17. Sema: “Ni nani ambaye aweza kukulindeni na Mwenyezi Mungu kama (Mungu) akikutakieni uovu, au (nani anayeweza kuzuia rehema yake kama) akikutakieni rehema?” Wala hawatapata mlinzi wala msaidizi kinyume cha Mwenyezi Mungu.

18. Bila shaka Mwenyezi Mungu Anawajua wale wanaojizua miongoni mwenu (wasende vitani pamoja na Mtume) na wawaambiao ndugu zao; “Njooni kwetu (wala msende kwa Muhammad);” wala hawendi katika mapigano ila kidogo tu (ili kuwadanganya Waislamu)

19. Wakakufanyieni choyo (kukusaidieni), lakini inapokuja hofu, utawaona wanakutazama, macho yao yanazungukazunguka kama yule aliyezimia kwa mauti; lakini hofu inapoondoka, wanakuudhini kwa ndimi zao kali, wanaifanyia choyo kheri, (hawataki kusaidia). Hao hawakuamini, kwa hivyo Mwenyezi Mungu Ameviondoshea thawabu vitendo vyao; na hayo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu.

20. (Mpaka sasa kwa woga wao) Wanafikiri yale makundi (ya maadui) hayajaondoka. Na kama makundi hayo yangukuja (tena), wangependa laiti wangukua wako jangwani pamoja na Mabedui,

26. Hao Mayahudi waliochanganyika na Makafiri wa Kiarabu ni katika kabila la Bani Quraidha ambao walikuwa na mapatano na Mtume kuwa waishi kwa amani na wasaidiane. Walipovunja ahadi hiyo, wakachanganyika na maadui na wakavunjikiwa, Mtume akawaendea katika ngome zao akawapiga, wengine akawaua na wengine akawafanya mateka.

بَيِّنَاتٍ مِّنَ الْكِتَابِ وَمَا هِيَ بِغُورَةٍ إِن يَشِئْ وَيَدُونَ إِلَّا فِرَارًا ۝

وَلَوْ دُخِلَتْ عَلَيْهِمْ مِّنْ أَقْطَارِهَا ثُمَّ سُيِلُوا
الْفِتْنَةَ أَتَوْهَا وَمَا تَلَبَّثُوا فِيهَا إِلَّا بَشِيرًا ۝

وَلَقَدْ كَانُوا عَاهِدُوا لَ اللَّهِ مِنْ قَبْلُ لَا يُؤْلَوْنَ
الَّذِينَ بَرَاءَ وَكَانَ عَهْدُ اللَّهِ مَسْئُولًا ۝

قَالَ لَنْ يَبْقَعَ لَكُمْ الْفِرَارُ إِن قُرَّرْتُمْ مِّنَ الْمَوْتِ
أَوْ الْقَتْلِ وَإِذَا لَا تَشْعُونَ إِلَّا قَلِيلًا ۝

قَالَ مَن ذَا الَّذِي يَعْصِيكُمْ مِّنَ اللَّهِ إِن أَرَادَ بِكُمْ
سُوءًا أَوْ أَرَادَ بِكُمْ رَحْمَةً وَلَا يَجِدُونَ لَهُمْ مِّنْ
دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ۝

قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الْمُعَوِّقِينَ مِنْكُمْ وَالْقَائِلِينَ
لِإِخْوَانِهِمْ هَلْ هُمْ الْيَنَاءُ وَلَا يَأْتُونَ الْبَاسَ إِلَّا
قَلِيلًا ۝

أَشْجَةً عَلَيْهِمْ ۖ فَإِذَا جَاءَ الْحَوْفُ رَأَيْتَهُمْ
يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ تَدُورُ أَعْيُنُهُمْ كَالَّذِي يُغْشَى
عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ۖ فَإِذَا ذَهَبَ الْحَوْفُ سَقُّوكُمُ
بِالْسِّنَةِ جِدَادٍ أَشْجَةً عَلَى الْخَيْرِ أُولَئِكَ
لَمْ يُؤْمِنُوا فَأَحْبَطَ اللَّهُ أَعْمَالَهُمْ ۖ وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى
اللَّهِ يَسِيرًا ۝

يَحْسَبُونَ الْأَحْزَابَ لَمْ يَذْهَبُوا ۖ وَإِنْ يَأْتِ الْأَحْزَابُ
يَوَدُّوا لَوْ أَنَّهُمْ بَادُونَ فِي الْأَعْدَابِ يَسْأَلُونَ

wakiuliza tu habari zenu. Na kama wanalikuwa pamoja nanyi wasingalipigana ila kidogo tu. (Mara wangelikimbia kwa woga wao).

21. Bila shaka mnao mfano mwema (ruwaza nzuri) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho, na kumtaja Mwenyezi Mungu sana.

22. Na Waislamu (wa kweli) walipoyaona majeshi (ya makafiri yamewashambulia hivyo), walisema, "Haya ndiyo Aliyotuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (kuwa tutapata misukosuko, kisha tutashinda). Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wamesema kweli;" na (jambo hili) halikuwazidishia ila imani na utii.

23. Wapo watu miongoni mwa walioamini waliotimiza ahadi waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu: Baadhi yao wamekwishamaliza umri wao, (wamekwisha kufa), na baadhi yao wanangoja (siku yao kufika), wala hawakubadilisha (ahadi yao) hata kidogo

24. Ili Mwenyezi Mungu Awalipe wakweli kwa sababu ya ukweli wao, na kuwaadhibu wanafiki Akipenda (kwa kuwa hawakurejea), au kuwageukia (kwa rehema kama wakitubia). Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

25. Na wale waliokufuru Mwenyezi Mungu Aliwarudisha na ghadhabu yao, hawakupata chochote katika heri; na Mwenyezi Mungu akawakifia Waislamu mapigano. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mbora.

26. Na Akawateremsha wale waliowasaidia (maadui) katika watu waliopewa Kitabu (kabla yenu; Mayahudi; aliwatoa) kutoka katika ngome zao, na Akatia khofu katika nyoyo zao, baadhi yao mkawa mnawaua, na wengine mnawateka.

27. Na Akakurithisheni nchi yao na majumba yao na mali zao, na nchi msiyoikanyaga (kabla ya hapo): Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

28. Ewe Mtume! Waambie wake zako: "Ikiwa mnapenda maisha ya (hii) dunia na uzuri wake (mimi si nayo, na mimi siwezi kukulazimisheni kukaa na mimi katika hali ya ufakiri; basi mkipenda nikuacheni), njooni, nitakupeni kitoka nyumba, (baadhi ya matumizi) na kukuacheni muwachano mzuri."

عَنْ أَنْبَاءِكُمْ دَلِيلًا كَانُوا فِيكُمْ مَا قَتَلُوا إِلَّا
قَلِيلًا ۝

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن
كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَ الْيَوْمَ الْآخِرَ وَ ذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ۝

وَ لَمَّا رَأَى الْمُؤْمِنُونَ الْأَحْزَابَ قَالُوا هَذَا مَا
وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَ صَدَقَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ
وَ مَا نَرَاهُمْ إِلَّا أَيْمَانًا وَتَسْلِيمًا ۝

مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ
عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَنْ قَضَىٰ نَحْبَهُ وَ مِنْهُمْ مَنْ يَنْتَظِرُ
وَ مَا بَدَّلُوا شَيْئًا ۝

يَلْبِغُونَ اللَّهُ الشُّدَّةَ بَصْدَقِهِمْ وَ يُعَذِّبُ
الْمُنَافِقِينَ إِنَّ شَاءَ أَوْ تَوْبَ عَلَيْهِمْ إِنَّ اللَّهَ
كَانَ غَفُورًا رَّحِيمًا ۝

وَ رَأَى اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِغَيْطِهِمْ لَمَّا رَأَى الْخَيْبَ وَ
كَفَىٰ اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ الْقِتَالَ وَ كَانَ اللَّهُ قَوِيًّا عَزِيمًا ۝

وَ أَنْزَلَ الَّذِينَ ظَاهَرُوهُمْ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مِنْ
صِيَالِهِمْ وَ قَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ فَرِيقًا تَقْتُلُونَ
وَ تَأْسِرُونَ فَرِيقًا ۝

وَ أَوْشَكْتُمْ أَصْهَهُمْ وَ دِيَارَهُمْ وَ أَمْوَالَهُمْ وَ أَرْضًا
لَّمْ تَطُوهَا وَ كَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرًا ۝

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لِّأَزْوَاجِكَ إِن كُنْتُمْ تُرِيدُونَ
الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَ زِينَتَهَا فَتَعَالَيْنَ أُمَتِّعْكُنَّ
وَ أُسَرِّحْكُنَّ سَرَاحًا جَمِيلًا ۝

29. Na kama mnamtaka Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na nyumba ya akhera, basi Mwenyezi Mungu Amewaandalia wafanyao mema hayo, miongoni mwenu, malipo makubwa.

30 Enyi wake wa Mtume! Atakayefanya maovu dhahiri miongoni mwenu, atazidishiwa adhabu mara mbili; na haya ni sahali kwa Mwenyezi Mungu.

31. Na miongoni mwenu atakayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na kutenda mema, Tutampa malipo yake mara mbili, na kumwandalia riziki yenye hishima.

32. Enyi wake wa Mtume, nyinyi si kama yoyote tu katika wanawake wengine. (Nyinyi wakeze Mtume). Kama mnataka (kufanya jambo la) kumcha Mwenyezi Mungu, basi msilegeze sauti (zenu mnaposema na wanaume) ili asitamani mtu mwenye ugonjwa moyoni mwake (kufanya mabaya na nyiye) na semeni maneno mazuri.

33. Na kaeni majumbani mwenu, wala msionyeshe mapambo yenu kama walivyokuwa wakionyesha mapambo yao wanawake wa zama za Ujahili (Ujinga, ukafiri) na simamisheni Sala na toeni Zaka, na Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Mwenyezi Mungu Anataka kukuondoleeni uchafu, enyi watu wa nyumba (ya Mtume), na (anataka) kukutakaseni kabisa kabisa.

وَأَنْ كُنْتُمْ تُرَدُّونَ إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَالْأَخِرَةَ
فَإِنَّ اللَّهَ أَعَدَّ لِلْمُحْسِنِينَ أَجْرًا عَظِيمًا ۝

يُنِسَاءَ النَّبِيِّ مَنْ يَأْتِ مِنْكُمْ بِفَاحِشَةٍ مُبَيَّنَةٍ
يُضَعَّفُ لَهَا الْعَذَابُ ضِعْفَيْنِ وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ
يَسِيرًا ۝

وَمَنْ يَقْنُتْ مِنْكُمْ لِلَّهِ وَرَسُولِهِ وَتَعَمَلْ صَالِحًا
تُوَفَّقْهَا أَجْرَهَا مَرَّتَيْنِ وَأَعْتَدْنَا لَهَا رِزْقًا كَرِيمًا ۝

يُنِسَاءَ النَّبِيِّ لَسْتُمْ كَأَحَدٍ مِنَ النِّسَاءِ إِنَّ الْأَقْيُسْنَ
فَلَا تَحْضَعْنَ بِالْقَوْلِ فَيَطْمَعَ الَّذِي فِي قَلْبِهِ
مَرَضٌ وَقُلْنَ قَوْلًا مَعْرُوفًا ۝

وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ
الْأُولَى وَأَقِمْنَ الصَّلَاةَ وَآتِينَ الزَّكَاةَ وَأَطِعْنَ اللَّهَ
وَرَسُولَهُ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ
أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ۝

30. Mambo yanatengeneza kwa wakubwa na yakaharibika kwa wakubwa. Wao ndio wanaofuatwa mwendo wao, ukiwa mwema au mbaya. Basi ndio wanaambiwa hapa wakeze Mtume — mabibi wa kuigwa — kuwa wakenda mwendo mbaya watalipwa kwa ukali zaidi kuliko wabaya wengine. Na wakenda mwendo mzuri watalipwa vizuri zaidi kuliko wema wengineo wote. Kila jambo linalipwa kwa kadiri ya athari yake.

31. Wakubwa kila siku ndio shabaha za wadogo katika kuwafuata. Wanalolifanya wakubwa ndilo linaloigwa; likiwa jema, likiwa baya, kwa kuwa watu wanaona kuwa hayo yanayofanywa na wakubwa ndio utamaduni, (ustarabu). Basi wanaiga; wajionyeshe kuwa na wao ni watamaduni waliotimu wasio na nukusani.

Ndio maana hao wakubwa wakajaziwa jaza kubwa kabisa za kheri wanapokwenda mwendo mzuri, kwani kwa njia hiyo wanaongoa chungu ya watu; na wapakewa ikabu kubwa zaidi wanapojipotoa kwani wengi wanawapotoa.

32. Ukubwa aliokupa Mwenyezi Mungu una zaka zake. Na moja katika zaka hizo ni kwenda mwendo mzuri, ikiwa si hivyo basi ikabu itakuwa kubwa. Na wanawake pambo lao kubwa kabisa ni kutua na kuchunga wao muruwa, wasiwe na chembe ya dowa wala towa. Na anayemuharibu mwanamke ni mwanamume. Shetani wa Binadamu ni Binadamu mwenziwe. Na mwanzo wa sababu ya kufanya maasi ya mwanamume na mwanamke ima kuonanana wakapendana au kusikia sauti wakaashikiana.

Ndio maana wanaambiwa wanawake hapa kuwa ikitokea dharura ya mwanamke kusemezana na mwanamume akaze sauti yake, asijesimeze kwa madaha; asije akavuutika huyo mwenziwe kutaka kufanya mabaya naye. Na walivyoambiwa haya wakeze Mtume ndio wanaambiwa wanawake wengine wote.

33. Basi kama walivyokatazwa katika ile Aya ya pili kuzisikilizisha sauti zao ndivyo katika Aya hii wanavyokatazwa kuonyesha (a) Miili yao, (b) Mapambo yao.

Wanaambiwa wakae majumbani mwao, wasitoke ovyo ovyo. Watoke kwa dharura na haja tu. Ikiwa si hivyo basi wajikalie majumbani mwao wachunge muruwa wao.